

Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482

JEHANAMU YA MOTO

Katika masomo yaliyopita tulijifunza kwamba nafsi hufa na haina uhai au haipo baada ya kifo. Leo tutajifunza habari ya kuzimu. Watu wengi huona kuzimu kuwa mahali pa moto pa adhabu ambapo nafsi zenye kutokufa, zisizokufa zinateswa milele. Wale wanaoamini hili wanasema sio tu kwamba mpango huu ulifanywa na Mungu, bali pia ni Mungu ndiye aliyemfanya Ibilisi kuwa "mlinzi wa kuzimu." Tunapotazama Neno la Mungu, tutaona kwamba hakuna hata moja kati ya haya ambayo ni ya kweli.

Karibu kila mtu anakubali kwamba wanadamu wote ni watenda dhambi na kwamba dhambi lazima iadhibiwe. Lakini adhabu ya haki kwa dhambi inahusisha nini? Chochote Mungu afanyacho tunajua kitakuwa haki kwa sababu haki ndiyo msingi wa kiti chake cha enzi: "*Haki na hukumu ndio msingi wa kiti chako cha enzi; upendo na uaminifu zitakutangulia*" (Zaburi 89:14 [1]).

Je, mtu anatakiwa kufanya apendavyo kwa kiasi gani katika siku? Yeye hutumia theluthi moja ya muda (siku) kulala, anafanya kazi kwa theluthi nyingine, na anaweza kupata muda wa kufanya shughuli zingine usiozidi theluthi moja. Ikiwa aliishi hadi umri wa *miaka tisini*, basi ingeweza kusemwa kuwa anatenda dhambi theluthi moja ya muda wake—*miaka thelathini*! Je, ni nini kinachojumuisha adhabu ya haki kwa dhambi zilizotendwa kwa muda wa miaka thelathini?

Hakika si miaka bilioni ya moto wa kuzimu, wala mabilioni ya bilioni ya miaka. Hakuna mtu angeita hii kuwa ni haki!

Mtume Paulo alituambia nini adhabu ya dhambi: "*Kwa maana mshahara wa dhambi ni **mauti***" (Warumi 6:23). Ingawa andiko hili halisemi chochote kuhusu kuzimu, tunajua neno hilo kuzimu linapatikana katika Agano la Kale na Agano Jipya. Kwa hivyo tunahitaji kuelewa kuzimu ni nini, na ni nani anayeenda kuzimu, na mtu atatokaje kuzimu.

Kuzimu katika Agano la Kale

Maana ya awali wa neno la Kiingereza kuzimu ilikuwa ni "kufunika au kuficha." Hivyo mkulima wa Kiskoti anaweza kusema, "inabidi nifukie(kuzimu) viazi vyangu" (vizike ardhini), au "inabidi niezeke(funike) nyumba yangu" (weka nyasi juu ya paa). Wakati fulani katika *zama za giza* neno hilo lilikuja kumaanisha "mahali pa mateso ambapo watu waovu huenda wanapokufa," jambo lililo tofauti kabisa na "kufunika au kuficha."

Neno "kuzimu" linapatikana mara hamsini na tatu katika Biblia ya *King James (KJV)*. Kati ya mara thelathini na moja ambapo neno "kuzimu" inaonekana katika Agano la Kale, chanzo cha neno la Kiebrania ni *sheol*. Neno hilo (*sheol*) pia limetafsiriwa "kaburi" mara thelathini na moja, na "shimo" mara tatu. Watafsiri waliamua kutumia maneno matatu ya Kiswahili ili kuwasilisha maana ya neno hilo moja la Kiebrania. Hata leo, tafsiri zinaonekana kupingana juu ya neno gani la Kiswahili la kutumia. Hapa kuna mfano mmoja: "*Waovu watarejezwa **kuzimu**, na mataifa yote wanaomsahau Mungu*" (Zaburi 9:17, *KJV*). "*Waovu hurudi **kaburini**, naam mataifa yote wanaomsahau Mungu*" (*NIV Bible*). Neno la Kiebrania *sheol* linatafsiriwa "kuzimu" na baadhi ya watafsiri, na wengine wanatafsiri "kaburi".

"*Wanawe wote [wa Yakobo] na binti zake wote wakaja kumfariji, lakini akakataa kufarijiwa. Hapana, alisema, kwa huzuni nitashuka mpaka **kaburini** kwa mwanangu*. (Mwanzo 37:35). "*Kwa maana **kuzimu** hakuwezi kukusifu, kifo hakiwezi kukuimbia; washukao shimoni hawawezi kuutumainia uaminifu wako*" (Isaya 38:18). Neno "kaburi" ni neno la Kiswahili la neno la Kiebrania *sheol*. Inaelezea **umauti (hali ya kifo)**.

Hivyo kuzimu katika Agano la Kale inarejelea "hali iliyofichika" ya kuzikwa, wala si mahali penye moto mkali. Hata hivyo, Ayubu anapotafakari kifo chake, anazungumza kuhusu hali ya giza kuu: "*Siku zangu chache hazijakaribia kwisha? … naenda … katika nchi ya giza kuu, ya uvuli wa giza na machafuko, ambapo hata nuru ni kama giza*" (Ayubu 20-22). **Umauti** ni mahali pa kimya: "*Sio wafu wamsifuo Bwana, Wale washukao mahali pa kimya*" (Zaburi 115:17). Ni sawa na hali ya kutokuwepo: "*Lolote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako zote, kwa maana huko **kaburini** [sheol], uendako wewe, hakuna kazi, wala shauri, wala maarifa, wala hekima*" (Mhubiri 9:10).

Mara kwa mara katika Agano la Kale neno la Kiebrania *sheol* linaelezea hali ya kifo (umauti) kama hali ya kukosa fahamu. Watafsiri wa *King James* wameficha utumizi huo thabiti kwa kutumia maneno matatu katika tafsiri yao ya Kiingereza: hell (kuzimu), grave (kaburi), na pit (shimo).

Kuzimu katika Agano Jipya

Maneno matatu ya Kigiriki katika Agano Jipya yametafsiriwa "kuzimu" na watafsiri wa *King James*: *hades, gehenna,* na *tartarus*. Neno *hades* linapatikana mara tisa na ni neno la Kigiriki linalolingana na neno la Kiebrania *sheol.* Inamaanisha tu hali ya wafu, yaani umauti. Tunaweza kuthibitisha hili kwa kulinganisha mstari kutoka katika Agano la Kale ambao umenukuliwa katika Agano Jipya: "*Hutaiacha nafsi yangu **kuzimu** [Kiebrania: sheol] wala hutamtoa Mtakatifu wako aone*

uharibifu" (Zaburi 16:10), *King James*). *"Hutaiacha nafsi yangu **kuzimu** [Kigiriki: hades], wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu"* (Matendo 2:27, *King James*). [2]Ni wazi kwamba neno la Kigiriki *hades* lina maana sawa na neno la Kiebrania *sheol* .

Tunaambiwa kwamba hata Yesu alienda kuzimu: *"[Daudi] akiona hayo, alitangulia kunena habari za ufufuo wa Kristo, ya kwamba nafsi yake haikuachwa **kuzimu**"* (Matendo 2:31). Yesu alikuwa kuzimu au *hades* kwa siku tatu. Hiyo ina maana kwamba alikuwa katika "umauti – hali ya kifo" hadi alipofufuliwa siku ya tatu. Ikiwa kuzimu au *hades* palikuwa mahali pa mateso, basi Yesu angeenda mahali ambapo angeteswa. Lakini ***kuzimu ya Biblia*** haiko hivyo hata kidogo. "Hakuachwa" katika *kuzimu* kwa sababu alifufuliwa kutoka katika hali ya kifo, yaani umauti. Kila mtu mwingine yeyote ambaye amekufa **ameachwa** katika hali ya kifo (umauti) hadi watakapofufuliwa katika ufalme wa Kristo.

Katika kitabu cha mwisho cha Biblia Yesu anatuambia kwamba ana *"funguo za **kuzimu** [hades] na za **mauti**"* (Ufunuo 1:18, *King James*). "Ufunguo" unawakilisha mamlaka ya kufungua mlango, katika kisa hiki "mlango wa fursa." Anasema ana mamlaka juu ya mauti (kifo) na kuzimu, na ni muhimu tufahamu tofauti kati ya hizo mbili, yaani mauti na kuzimu

Katika tukio moja Yesu alisema: "*Waache wafu wazike wafu wao*" (Luka 9:60). Wale wasio hai katika Kristo wanahesabiwa kuwa wamekufa mbele za Mungu, ingawa bado wanaishi na wanapumua. Hawa ndio wa kuwazika wale ambao hawapo hai na hawapumui. Hivyo Ufunguo #1 unawakilisha mamlaka ya Yesu juu ya "wafu" walio hai/wanaopumua wa ulimwengu. Ufunguo #2 unawakilisha

---

[2]Kumbuka: Wafasiri wa *NIV* walichagua neno "kaburi" badala ya "kuzimu" katika vifungu vyote viwili.

mamlaka yake juu ya wale walio katika nyumba ya gereza ya mauti, wale ambao wamekufa kabisa, yaani hawapumui. Mungu alimpa Yesu mamlaka ya kuondoa hukumu ya kifo iliyo juu ya walio hai na wafu pia. Na Petro anathibitisha hili: "*Yeye [Yesu] ndiye aliyewekwa na Mungu awe mhukumu wa walio hai na wafu*" (Matendo 10:42).

Andiko moja la mwisho linalotumia neno *hades* lafaa kuzingatiwa: "Bahari ikawatoa wafu waliokuwa ndani yake; na mauti na **kuzimu** [*hades*] vikatoa wafu waliokuwa ndani yake … na mauti na **kuzimu** [*hades*] vikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili." (Ufunuo 20:13,14, *King James*). "Kuzimu" inasemekana "kuwatoa wafu" iliyokuwa nao. Na kisha, "mauti na kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto." Baada ya kuzimu (hali ya kifo) kuondolewa kwa wale wote waliokufa kupitia ufufuo, inaharibiwa katika "ziwa la moto," ishara inayofaa ya uharibifu kamili. Uharibifu huu hutokea katika ufalme wa Kristo wakati wafu wote watafufuliwa (taz. 1 Wakorintho 15:22).

Neno la pili la Kiyunani lililotafsiriwa kuzimu ni *gehenna* na linaonekana mara kumi na mbili. Mara tatu kati ya hizo hutokea katika nukuu hii: "Mkono *wako* ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima, u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehenum [gehenna] kwenye moto usiozimika; ambapo funza wao hawafi, na moto hauzimiki. Na mguu wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima ukiwa kilema, kuliko kuwa na miguu miwili na kutupwa katika *jehanum***,** katika moto usiozimika, ambamo funza wao hawafi. na moto hauzimiki. Na jicho lako likikukosesha, ling'oe; ni afadhali kuingia katika ufalme wa Mungu, ukiwa na jicho moja, kuliko kuwa na macho mawili na kutupwa katika **jehanum ya** *moto*, ambako funza wao hawafi, wala moto hauzimiki." (Marko 9:43-48 , *King James*).

Kwa kuwa hatujui hata kisa kimoja ambapo mtu yeyote alifanya hivyo kihalisi katika wakati wa Bwana wetu, tunaweza kuwa na hakika kwamba hadhira walielewa kwamba Yesu alikuwa akizungumza nao kwa njia ya mafumbo. Hakutumia neno la Kigiriki *hades*. Neno ni *jehanamu (gehenna)* na palikuwa mahali halisi. Katika Kiebrania neno "gehenna" linamaanisha Bonde la Hinnomna katika siku za Yesu lilikuwa ni dampo la jiji. Ndani yake zilitupwa takataka na nyama iliyokufa (mbwa, panya, na hata miili ya wahalifu waliouawa). Moto ulipunguza takataka nyingi kuwa majivu. Nyama iliyokufa isiyochomwa ilitoa minyoo(funza) iliyoila. Bila shaka wakati hakukuwa na kitu zaidi cha kuchoma, moto ulizima. (Hakuna hata kimoja leo hii.) Kulipokuwa hakuna tena nyama iliyokufa, minyoo ilitoweka. Moto na minyoo huashiria uharibifu kabisa. Hivyo tunaona kwamba hii "kuzimu/jehanamu" [*gehenna*] si sawa na "kuzimu" [*hades*] tuliyokuwa tukiijadili hivi punde.

Yesu aliporejelea "mkono" unaokosesha, alikuwa akiutumia kama ishara ya urafiki: "Amerika imeunga mkono Urusi. Kuunga mkono katika urafiki wa dhambi na ulimwengu unakuwa kikwazo kwa maendeleo ya Kikristo na hivyo mkono huo au urafiki huo unapaswa "kukatiliwa mbali." Urafiki mwingi tulio nao tunapopokea kweli, ikiwa utaendelea na kutiwa moyo, ungezuia sana ukuaji wa tabia ya Kristo. Urafiki wa ulimwengu huongeza "roho ya udunia" na hupunguza "roho mtakatifu." Urafiki wote usiofaa unapaswa "kukatiliwa mbali."

Yesu aliporejelea "mguu" unaokosesha, alikuwa akiutumia kama ishara ya mahali ambapo miguu yetu inaweza kutupeleka ambako kungekuwa vizuizi kwenye ukuaji wetu wa Kikristo. Hizi ni pamoja na michezo ya kamari ikijumuisha kamari kwenye matokeo ya michezo na mbio, baa, matumizi ya dawa za kulevya na jambo lolote ambalo tunajua Mungu hakubaliani nalo. Tunapaswa "kukatilia

mbali" sehemu yoyote ambayo inachochea udunia na kuzuia maendeleo ya Kikristo.

Yesu aliporejelea “jicho” lenye kuudhi, alikuwa akilitumia kama ishara ya kile tunachoona ambacho kinazuia maendeleo kama ya Kristo. Hayo yanahusisha magazeti, vitabu, na hasa **televisheni** yenye programu zake nyingi zenye kukengeusha. Haya hutumia muda wenye thamani na kutia moyo roho ya udunia ya ubinafsi katika moyo na akili. Ni lazima "tuwang'oe" ili kuzizuia zisiwe tabia.

Wakristo ni tofauti na wale walio katika ulimwengu huu: “*Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu, ambazo mlikuwa mkiishi humo mlipoifuata njia za ulimwengu huu. … Lakini kwa upendo wake mkuu kwetu sisi, Mungu, ambaye ni mwingi wa rehema, alituhuisha pamoja na Kristo, tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu*” (Waefeso 2:1,2,4,5). Mkristo hapaswi kamwe kuzirudia njia za ulimwengu huu kwa sababu ikiwa atafanya hivyo, na akiendelea kuukataa upendo mkuu wa Mungu, atakufa, si kifo kinachofafanuliwa na *kuzimu(hades)*, bali kifo cha pili, kinachofafanuliwa na *jehanamu (gehenna)*. Hakuna ukombozi kutoka kwa kwemye mauti hiyo ya pili, mauti ambayo inaofananishwa na “moto na funza.”

Hapa ni mfano mwingine: “**Msiwaogope** wauuao mwili, lakini hawawezi kuiua *nafsi*; bali mwogopeni yule awezaye kuangamiza nafsi na mwili pia katika jehanamu.” Hii inaelezea uangamivu kamili **na sio** kuhifadhiwa mahali pa mateso. Waovu wataangamizwa kwenye mwisho wa ufalme: “*Waoga, na wasioamini, na wachafu, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, mahali pao patakuwa katika ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya **pili.”*** (Ufunuo 21:8). Mauti ya pili inamaanisha kwamba walikufa hapo awali, kisha wakarudishwa kwenye uhai tena. Ikiwa basi watathibitika kuwa watenda-dhambi kimakusudi katika upinzani wao kwa Mungu na uadilifu, watakufa tena, yaani mara ya pili na hii

ndio sababu inaitwa mauti ya pili, yaani kufa kwa mara ya pili. hakutakuwa na ufufuo kutoka katika "kifo hiki cha pili – mauti ya pili" .

Adhabu ya Mungu kwa dhambi daima ni kifo/mauti (taz. Warumi 6:23). "*Ijapokuwa neema huonyeshwa kwa waovu, hawajifunzi haki; hata katika nchi ya unyofu wanaendelea kutenda maovu, wala hawauangalie utukufu wa BWANA* " (Isaya 26:10).

Neno la tatu la Kigiriki lililotafsiriwa kuzimu ni *tartarus* na linaonekana mara moja tu: "Mungu hakuwaachilia malaika walipofanya dhambi, bali aliwapeleka kuzimu [*tartarus*], akiwaweka katika shimo la giza ili walindwe hata ije hukumu" (2 Petro 2:4) Ona kwamba hii haisemi chochote kuhusu wanadamu. Inaeleza kilichowapata malaika waliotenda dhambi. *Tartaro* ni jina linalohusishwa na mahali ambapo malaika wenye dhambi walihifadhiwa. Eneo lake halijabainishwa, lakini wengine wanakisia kwamba walifukuzwa kutoka mbinguni hadi kwenye angahewa ya dunia. Hili linaweza kuwa jambo ambalo mtume Paulo alikuwa akifikiria alipoandika: "*Kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa ulimwengu huu wa giza*" (Waefeso 6:12).

Katika hili, mahali pekee katika Biblia panapozungumza juu ya kile kilichowapata malaika walioanguka, tunaambiwa uhuru wao ulikuwa na vikwazo vikali. Hawafurahii tena ulimwengu usio na mwisho wa Mungu kama walivyokuwa hapo awali. Maneno "shimo la giza" yanatukumbusha jambo ambalo Isaya aliandika: "*Giza limeifunika dunia na giza kuu liko juu ya mataifa*" (Isaya 60:2). Mapema katika barua yake kwa Waefeso Paulo alimwita Shetani "*mtawala wa ufalme wa anga*" (Waefeso 2:2).

Adhabu ya Mungu SI Mateso

Hapa kuna Maandiko machache zaidi ambayo yanasema wazi kwamba adhabu ya mwisho kwa watenda mabaya ni kifo bila uwezekano wa ufufuo. Sio mateso au kuendelea kuwepo kwa aina yoyote katika mazingira mbadala.

“*Watu waovu **watakatiliwa mbali,** bali wale wanaomngojea BWANA watairithi nchi. Bado kitambo kidogo asiye haki **hatakuwapo tena**; ukiwatafuta, hawataonekana*” (Zaburi 37:9,10).

“*BWANA huwaangalia wote wampendao, bali waovu wote **atawaangamiza** ”* (Zaburi 145:20).

“*Walio mbali nawe **wataangamia**; unawaangamiza wote **wasio** waaminifu kwako*” (Zaburi 73:27).

Maandiko hayo na mengine yanasema kwamba adhabu ya Mungu kwa waovu ni **uangamivu** na si kuhifadhiwa katika mateso. Lakini wengine wanafikiri tofauti, labda kwa sababu ya maneno haya: “Ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa liwakalo moto na kiberiti, ambamo yule mnyama na yule nabii wa uongo walikuwa wametupwa. Watateswa mchana na usiku milele na milele.” (Ufunuo 20:10). Lakini kumbuka: "ziwa hili liwakalo moto na kiberiti" hupokea mnyama mmoja, **nabii** wa uongo mmoja na **shetani** mmoja**.** Hakuna **watu** katika ziwa hili! Andiko hili halisemi chochote kuhusu hatima ya wasio haki.

Kabla ya kumalizia somo hili, na tuangalie kifungu kimoja zaidi: “Malaika zake … wataondoa katika ufalme wake kila kitu kinachosababisha dhambi na wote watendao maovu. Watawatupa katika tanuru ya moto, ambako kutakuwa na kilio na kusaga meno.” (Mathayo 13:41,42). Maneno yanayofanana na haya yanaonekana sehemu nyingine nne katika Mathayo na pia katika Luka 13:28.

tambua kwamba hakuna kinachosemwa kuhusu kuzimu. Maneno haya yanapaswa kueleweka kuwa ni mafumbo.

"Tanuru ya moto" ni mfano wa hukumu za haki za Mungu: "*BWANA anakuja na moto, na magari yake ya vita ni kama tufani; ataishusha hasira yake kwa ghadhabu, na lawama yake kwa miali ya moto. Maana kwa moto na kwa upanga wake BWANA atafanya hukumu juu ya watu wote, na wengi watakuwa waliouawa na BWANA*" (Isaya 66:15,16). Hilo larejelea hukumu za mwisho kwenye mwisho wa ulimwengu huu mwovu wa sasa, hukumu ambazo zitaharibu mifumo yote isiyo ya haki: "*Hakika siku ile inakuja; itawaka kama tanuru. Wote wenye kiburi, na kila mtenda mabaya watakuwa makapi, na siku hiyo inayokuja itawateketeza kwa moto, asema BWANA wa majeshi*" (Malaki 4:1).

Petro anathibitisha hili: *"Siku ya Bwana itakuja kama mwivi. Mbingu zitatoweka kwa kishindo; elementi zitaharibiwa kwa moto, na dunia na vyote vilivyomo ndani yake vitawekwa wazi*" (2 Petro 3:10).

Maneno "kulia na kusaga meno" yanaelezea majuto makubwa. Yesu aliwaambia Mafarisayo: "*Huko kutakuwa na kilio na kusaga meno, wakati mtakapowaona Abrahamu, Isaka na Yakobo na manabii wote katika ufalme wa Mungu, lakini ninyi wenyewe mmetupwa nje*" (Luka 13:28). Yesu aliwaambia viongozi wa Kiyahudi kwamba katika ufalme ujao duniani hawangekuwa na mamlaka ya ofisi waliyokuwa wakifurahia wakati huo na ingesababisha majuto makubwa kwa upande wao.

Kwa hakika sasa kwa kuwa tunaelewa kwamba ***kuzimu ya Biblia*** inamaanisha umauti (hali ya kifo) na si mateso, twaweza kumwona Mungu wetu jinsi alivyo: mwenye upendo, haki, na ambaye ni mwenye haki katika kutendea uumbaji wake wa kibinadamu. "*Hakika kama niishivyo, asema Bwana MUNGU, sifurahii kufa kwao watu mwovu, bali waziache njia zao na kuishi*" (Ezekieli 33:11). "*Sifurahii kifo cha yeyote, asema Bwana Mwenye Enzi Kuu Yehova. Tubuni na uishi*!" (Ezekieli

18:32). Biblia inatuambia kwamba Mungu hafurahii kifo cha mtu yeyote na hivyo ndivyo tu tungetarajia kutoka kwa Mungu wa upendo.

Utukufu uwe kwa Mungu kwa ajili ya nuru ya ukweli juu ya somo hili.

-Amina-



Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:

Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com

©HAKIUZWI

Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482